

**HALMASHAURI YA WILAYA YA UKEREWE  
MKOA WA MWANZA**

Simu+255 732 981174/+255 737 1782  
Fax: +255 732 981174/+255 28 25150

Email: ukerewedc@yahoo.com  
Ukijibu tafadhalii taja



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W),  
S.L.P. 41,  
**NANSIO/UKEREWE.**

Kumb. Na.GA.30/95/01/66

03/04/2018

**YAH: TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI.**

Kwa Mujibu wa Kibali cha Ajira Kumb. Na. CFC 26/205/01'FF'/91 cha tarehe 22 Agosti, 2017 kama kilivyoongezwa muda kibali Kumb.Na. CFC 26/205/01'GG'/95 cha tarehe 12 Machi, 2018 kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe anawatangazia Watanzania wote wenye sifa na uwezo wa kuajiriwa kutuma maombi ya kazi ifuatayo;:-

**AFISA MTENDAJI WA KIJIJI DARAJA LA III (NAFASI 40).**

**1. SIFA ZA MWOMBAJI.**

Kuajiriwa wenye Elimu ya Kidato cha Nne (IV) au Sita (VI), aliyehitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti (TECHNICAL CERTIFICATE NTA- LEVEL 5) katika moja ya fani zifuatazo;- Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

**2. KAZI/MAJUKUMU.**

- i) Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji.
- ii) Kusimamia ulinzi na usalama wa Raia na Mali zao, kuwa mlinzi wa amani kusimamia utawala Bora katika Kijiji.
- iii) Kuratibu na kusimamia upangaji na utekekelezaji wa mipango ya Maendeleo katika Kijiji.
- iv) Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji.
- v) Kutafsiri na Kusimamaia Sera, Sheria na Taratibu.
- vi) Kuandaa taarifa za Utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa umaskini na kuongezauzalishaji mali.
- vii) Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya Kitaalam katika Kijiji.
- viii) Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za Kijiji.
- ix) Mwenyekiti wa kikao cha Wataalam waliopo katika Kijiji.
- x) Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko, kero na migogoro ya Wananchi.
- xi) Kusimamia utungaji wa Sheria ndogo za Kijiji.
- xii) Atawajibika kwa Afisa Mtendaji wa Kata.

### 3. NGAZI YA MSHAHARA.

Cheo cha Afisa Mtendaji wa Kijiji Drj III kina ngazi ya Mshahara wa TGS B, yaani Tshs. 390,000/= kwa mwezi.

### 4. MASHARTI KWA UJUMLA.

- i) Mwombaji awe ni raia wa Tanzania asiezidi umri wa miaka 45.
- ii) Mwombaji awe hajawahi kupatikana na kosa lolote la jinai, kufungwa jela au kupatikana na kosa lolote katika Utumishi wa Umma.
- iii) Mwombaji aambatanishe taarifa zake binafsi (CV) ikionyesha sanduku la posta, E-mail, namba za simu anazotumia na uzoefu wake kazini.
- iv) Maombi yote yaambatanishwe na nakala za vyeti vya taaluma, vyeti vya kidato cha nne (IV) au sita (VI), cheti cha kuzaliwa na picha mbili (*Passport size*) za hivi karibuni.
- v) Nakala zote za vyeti zithibitishwe na Hakimu au Mwanasheria aliyesajiliwa na kuthibitishwa.
- vi) Maombi yote yaandikwe kwa mkono.
- vii) Testimonials, statement of results, hati ya matokeo ya kidato cha nne na sita na provisional results **HAZITAKUBALIKA**.
- viii) Kwa waombaji waliosoma nje ya nchi, wawasilishe uthibitisho wa vyeti vyao kutoka Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA), na kwa waliohitimu vyuo nje ya nchi pia wawasilishe uthibitisho wao kutoka Baraza la Elimu ya Ufundji la Taifa (NACTE).
- ix) Kwa watakaochaguliwa kuhudhuria usaili watajulishwa kuitia namba za simu walizoweka kwenye barua zao za maombi pamoja na anuani zao za posta.
- x) Maombi yasiyozingatia vigezo viflyoainishwa hapo juu **HAYATASHUGHULIKIWA**.
- xi) Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 18/04/2018 saa 9:30 alasiri.

**MUHIMU;**- Barua za maombi zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji (W), kuitia anuani ifuatayo;-

Mkurugenzi Mtendaji (W),  
Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe,  
S.L.P 41,  
**NANSIO/UKEREWE**

Pia tangazo hili linapatikana kuitia tovuti ya Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe  
[www.ukerewedc.go.tz](http://www.ukerewedc.go.tz)

*Bhati*

Frank S.Bahati

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**  
**UKEREWE**

Nakala;- i) Jalada GA.30/95/01/66  
ii) Mbao zote za Matangazo.

*MKURUGENZI MTENDAJI (W)*  
*UKEREWE*